


**East African Journal of Arts and Social Sciences**
eajass.eanso.org
**Volume 8, Issue 1, 2025**
**Print ISSN: 2707-4277 | Online ISSN: 2707-4285**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-4285

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Tathmini ya Mchango wa Tafsiri Katika Maendeleo ya Fasihi Linganishi

*Hadija Jilala*[1*]

[1] The Open University of Tanzania, P. O. Box. 23409, Dar es Salaam, Tanzania.
[*] Author's Email: hadija.jilala@out.ac.tz

**Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652**

**Date Published:**

*29 January 2025*

**Keywords**:

*Tafsiri,*
*Fasihi Linganishi,*
*Tathmini,*
*Maendeleo.*

## ABSTRACT

Makala hii inatathmini mchango wa tafsiri katika maendeleo ya fasihi linganishi. Tafsiri ni daraja la mawasiliano na utangamano wa jamii zinazozungumza lugha tofauti na zenye tamaduni tofauti. Tangu awali, kazi za fasihi za lugha mbalimbali zilitafsiriwa kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. Kupitia tafsiri hizo, jamii mbalimbali ulimwenguni hupata maarifa na ufahamu kuhusu maisha, tamaduni, lugha na fasihi ya jamii nyingine. Kutokana na uhalisia huo makala hii inalidurusu suala la tafsiri na fasihi linganishi kwa kutathmini mchango wa tafsiri katika maendeleo ya fasihi linganishi. Lengo la makala hii ni kutathmini mchango wa tafsiri katika maendeleo ya fasihi linganishi ya Kiswahili. Makala hii inajadili umuhimu wa tafsiri katika kufanikisha ulinganishaji wa kazi za fasihi na pia inajadili matatizo ya tafsiri katika fasihi linganishi. Utafiti huu ni wa maktabani ambapo data za makala zake zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini. Aidha, nadharia ya hii imetumia nadharia ya ulinganifu wa kidhima katika kujadili na kufafanua data na matokeo ya utafiti huu. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kuwa tafsiri ina mchango mkubwa katika maendeleo ya fasihi linganishi kwa sababu ni vigumu kuliganisha fasihi ya lugha ya jamii fulani bila kuitafsiri. Hivyo, tafsiri ni nyenzo na msingi madhubuti wa kuelewa fasihi za jamii nyingine na pia ni daraja muhimu la ufahamu na utambuzi wa kufanana, kuhusiana na kutofautiana kwa fasihi za lugha na tamaduni mbalimbali duniani.

**APA CITATION**

Jilala, H. (2025). Tathmini ya Mchango wa Tafsiri Katika Maendeleo ya Fasihi Linganishi. *East African Journal of Arts and Social Sciences*, *8*(*1*), 128-144. https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

**CHICAGO CITATION**

Jilala, Hadija. 2025. "Tathmini ya Mchango wa Tafsiri Katika Maendeleo ya Fasihi Linganishi". *East African Journal of Arts and Social Sciences* 8 (1), 128-144. https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652.

**HARVARD CITATION**

Jilala, H. (2025) "Tathmini ya Mchango wa Tafsiri Katika Maendeleo ya Fasihi Linganishi". *East African Journal of Arts and Social Sciences*, 8(1), pp. 128-144. doi: 10.37284/eajass.8.1.2652.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

**IEEE CITATION**

H., Jilala "Tathmini ya Mchango wa Tafsiri Katika Maendeleo ya Fasihi Linganishi". *EAJASS*, vol. 8, no. 1, pp. 128-144, Jan. 2025.

**MLA CITATION**

Jilala, Hadija "Tathmini ya Mchango wa Tafsiri Katika Maendeleo ya Fasihi Linganishi". *East African Journal of Arts and Social Sciences*, Vol. 8, no. 1, Jan. 2025, pp. 128-144, doi:10.37284/eajass.8.1.2652.

## INTRODUCTION

Shughuli za kutafsiri kazi za fasihi zilianza zamani kama tulivyoona hapo awali. Kwa mfano, Lun, (2018) anaeleza kuwa tafsiri ya kazi za fasihi iliyofanywa na Lin Shu, kama vile *The Lady of Camellias*, *The Cabin of Uncle Tom* ilikuza upeo wa kusoma na kuandika kwa Kichina na ilichangia katika ukuaji na maendeleo ya riwaya za kisasa za Kichina. Lun, pia anatoa mfano wa Zhu Shenghao, ambaye alijitolea kutafsiri kazi za Shakespeare. Anaeleza mwaka 1935, Zhu alianza kutafsiri kazi za Shakespeare, na katika miaka kumi iliyofuata, alikuwa tayari ametafsiri juzuu 27. Tafsiri zake zilisaidia kumtambulisha kwa wasomaji wa Kichina mwandishi mkubwa na maarufu wa tamthiliya duniani Shakespeare kutoka Uingereza na pia kuimarisha fasihi ya Kichina. Vilevile, Mehrpouyan na mwenzake (2021:18) wanaeleza kuwa nyimbo za Shakespeare zilipata umaarufu nchini Iran baada ya Omid Tabibzadeh kuzitafsiri katika Kiajemi na pia tafsiri ya Hamlet na M. E. Behazin.

Kwa ujumla, jamii na mataifa mengi duniani yamepiga hatua kubwa ya maendeleo kutokana na kubadilishana maarifa, ujuzi na taarifa. Aidha, katika siku za hivi karibuni utandawazi wa kiutamaduni umeshika kasi kubwa ulimwenguni ambapo jamii mbalimbali zimeweza kutangamana, kuhusiana na kuhamisha utamaduni na maarifa kutoka jamii moja kwenda jamii nyingine. Tunaweza kusema kuwa tafsiri imechukua nafasi kubwa sana katika kufanikisha utangamano, kusambaza ujuzi na maarifa ya kitaaluma na kiutamaduni ulimwenguni (Carlos, 2012). Aidha, Kelly (1979:1) anaeleza kwamba Ulaya Magharibi ilifaidi ustaarabu na maendeleo kutokana na juhudi za mfasiri. Naye, Momanyi (2017:1) anaongezea kuwa, mafanikio ya himaya na tawala mbalimbali duniani yaliwezeshwa na tafsiri. Kwa mfano, Himaya ya Roma iliweza kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya kitaaluma, kibiashara na kiutawala kutokana na taaluma ya tafsiri. Anaendelea kueleza kuwa, utamaduni wa Kirumi uliathiriwa na ule wa Kiyunani kupitia tafsiri. Aidha, inasadikika kuwa Pythagoras hakuasisi uhakiki wake wa kimantiki hadi alipozuru Afrika. Anaongezea kuwa, Wamisri walikuwa na utaalamu wa hisabati, unajimu na sayansi kabla hata ya nyakati za Pythagoras. Katika muktadha huo, hata Plato alizuru Misri, barani Afrika ili kupata maarifa ya kifalsafa. Bila shaka uelewa na ufahamu wa wanazuoni hawa ulichangiwa zaidi na tafsiri.

Utamaduni wa mataifa mbalimbali ulimwenguni umeweza kuathiriwa kutokana na tafsiri. Momanyi (2017:1) anasema kuwa, hadi kwenye karne ya 19, utamaduni wa Ulaya ulikuwa umeathiriwa sana na tafsiri za lugha za Kiyunani na Kilatini. Anaendelea kueleza kuwa, utamaduni wa Kijerumani uliweza kuathiriwa kwa kiasi na fasihi ya William Shakespeare wa Uingereza. Pia kwenye karne hiyo ya 19, tamaduni nyingi za Kiafrika ziliathiriwa na tamaduni za Ulaya hasa kupitia tafsiri za kifasihi kutoka katika lugha za Kimagharibi kwenda katika lugha za Kiafrika, ikiwemo lugha ya Kiswahili. Hivyo, ni dhahiri kuwa tafsiri imechangia ukuzaji wa maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali duniani. Kupitia tafsiri watu wamejifunza kuhusu fasihi za lugha zingine duniani, uzoefu, maisha na ustaarabu wao.

Katika eneo la Afrika Mashariki, historia inatuonesha kwamba harakati za kufasiri kazi za fasihi zilikuwa zikifanyika tangu Karne ya 18. Baadhi ya wahakiki wa fasihi ya Kiswahili kama vile Knappert (1979) wameeleza kwamba tafsiri ya maandishi katika fasihi ya Kiswahili ilianza mwaka wa 1749 wakati ambapo utenzi wa Kiarabu uliojulikana kama *Umm-ul Qura* ulitafsiriwa kwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

Kiswahili na Aidarus bin Athman na kujulikana kama *Utenzi wa Hamziyya*. Pia katika karne za 19 na 20 nazo zilishuhudia ufasiri wa kazi nyingi za fasihi za kigeni kwa lugha ya Kiswahili kama vile *Hekaya za Abunwasi na Hadithi Nyingine*, *Alfu-Lela-Ulela* (siku elfu na moja), *Hadithi za Esopo*, *Safari za Guliva*, *Robinson Kruso na Kisiwa chake* na *Elisi katika Nchi ya Ajabu*, miongoni mwa nyingine. Baada ya uhuru, kazi ya tafsiri iliendelea na zilifanyika tafsiri za vitabu vya William Shakespeare kama vile *Juliasi Kaizari* na *Mabepari wa Venisi*, kazi ambazo zilitafsiriwa na Mwalimu Julius Nyerere (1969). Jitihada za kutafsiri kazi fasihi ziliendelea hata katika vipindi mbalimbali vya maendeleo.

Hivyo, tafsiri ilitumiwa wakati wa ujio wa wageni kutafsiri kazi zao za fasihi na pia kutafsiri kazi za fasihi za wenyeji wao. Tendo la tafsiri liliwasaidia wageni kurithisha tamaduni zao, kujifunza na kufundisha lugha na utamaduni wa jamii. Baadhi ya kazi zilizotafsiriwa kwa Kiswahili ni: *Oedipus The King* 'Mfalme Edipode' (Sophocles), *Antigone* 'Antigoni' (Sophocles), *Merchant of Venice* 'Mabepari wa Venisi' ( Shakespeare), *The Government Inspector* 'Mkaguzi Mkuu wa Serikali' ( Gogol) na *Animal Farm* 'Shamba la Wanyama' ( Orwell). Vilevile zipo kazi fasihi ambazo zilitungwa na kuandikwa kwa lugha za kigeni kwa kuzingatia utamaduni na mazingira ya wenyeji wa Afrika. Miongoni mwa kazi hizo ni: *Things Fall Apart* 'Shujaa Okonkwo' (Achebe, 1958), *The Trials of Brother Jero* 'Masaibu ya Ndugu Jero' (Soyinka, 1963), *Arrow of God* 'Mshale wa Mungu' (Achebe, 1964), *The Black Hermit* 'Mtawa Mweusi' (Ngugi, 1968), *A Man of the People* 'Mwakilishi wa Watu' (Achebe, 1968), *Dying in the Sun* 'Kivuli Kinaishi' (Palangyo,1968), *The Beautiful Ones Are Not Yet Born* 'Wema Hawajazaliwa' (Armah, 1969), *The Burdens* 'Mizigo' (Ruganda, 1972), *Betrayal in the City* 'Usaliti Mjini' (Imbuga, 1976) na *The Trials of Dedan Kimathi* 'Mzalendo Kimathi' (Ngugi na Mugo, 1972).

Hivyo, tafiti na machapisho mbalimbali yameonesha kuwa tafsiri ni daraja ambalo liliwezesha na kufanikisha maendeleo ya jamii mbalimbali ulimwenguni. Tafsiri pia imesaidia kusambaa na kuenea kwa maarifa ya kitaaluma, kiutamaduni, lugha na fasihi za jamii mbalimbali kutoka jamii moja kwenda jamii nyingine (Ma Xiaolu, 2024). Umuhimu wa tafsiri katika fasihi linganishi umejadiliwa na kudhihirishwa na watafiti na wanazuoni mbalimbali baadhi yao ni; Lun, (2018); Surjeet, (2018); Huanga, (2022); Li,( 2022); Jahan, (2023); na Ma Xiaolu, (2024). Aidha, Munday, (2016: 44) anasisitiza kwamba, taaluma ya tafsiri ni taaluma ambayo imepanuka katika miaka ya hivi karibuni, na ina uhusiano wa msingi na taaluma za isimu, fasihi linganishi na utamaduni. Licha ya wataalamu hao kuonesha kuwa tafsiri ina uhusiano na fasihi linganishi, suala hilo bado halijafanyiwa uchunguzi na kujadiliwa ipasavyo.

Hata hivyo, mchango wa tafsiri katika fasihi linganishi ya Kiswahili ni jambo ambalo halijafanyiwa uchunguzi na kujadiliwa ipasavyo. Hivyo, tuliona kuna haja kuziba pengo hili kwa kufanya utafiti ili kuthathmini mchango wa tafsiri katika fasihi linganishi ya Kiswahili. Swali ambalo tunajiuliza ni je, tafsiri ina mchango gani katika maendeleo ya fasihi linganishi ya Kiswahili? Swali hili lilichochea haja ya kutathmini mchango wa tafsiri katika maendeleo ya fasihi linganishi ili kuona ni kwa namna gani tafsiri imechangia katika maendeleo ya fasihi linganishi ya Kiswahili. Kwa hiyo, makala hii imelenga kujadili umuhimu wa tafsiri katika fasihi linganishi na kuibua changamoto za kulinganisha kazi zilizotafsiriwa katika fasihi linganishi. Makala hii ina umuhimu mkubwa kwa sababu itasaidia kuonesha uhusiano wa taaluma ya tafsiri na fasihi linganishi ambayo kwa uhalisia ni taaluma mbili ambazo zinategemeana. Vilevile, itatoa mchango mkubwa katika taaluma ya tafsiri na fasihi linganishi.

Kimsingi, tunatambua kuwa, tafsiri inasaidia katika kutafsiri kazi za fasihi za lugha mbalimbali duniani. Kazi hizo zinapotafsiriwa huweza kulinganishwa na

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

kazi za fasihi za lugha ya jamii nyingine. Ulinganishaji huweza pia kufanywa na mtu ambaye anazifahamu lugha zote mbili yaani lugha chanzi na lugha lengwa na kutumia ujuzi wake wa lugha zote mbili kulinganisha kazi hizo (Baaqeel, 2018). Katika makala hii tumejikita kujadili kazi za fasihi ambazo zimetafsiriwa kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine.

Kwa muktadha huu upo uwezekano kuwa kazi zilizotafsiriwa kutoka lugha za kigeni kwenda Kiswahili zimechangia katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili kwa upande fulani au zimechochea changamoto katika fasihi hiyo kwa upande mwingine. Hii ni kwa sababu kupitia tafsiri ilikuwa rahisi kuelewa lugha, utamaduni, mila, desturi, kanuni na kaida za wageni na pia za wenyeji (Bassnett, 2018; Baaqeel, 2018; Huanga na mwenzanke., 2022; Jilala, 2023). Hivyo basi, kukosekana kwa ubayana wa mchango wa tafsiri katika fasihi ya Kiswahili ndiko kulikochochea nia ya kuandika makala hii ili kutathmini mchango wa tafsiri katika maendeleo ya fasihi linganishi ya Kiswahili na kuonesha jinsi tafsiri inavyochangia katika ulinganishaji wa kazi za fasihi duniani.

## DHANA YA TAFSIRI

Tafsiri ni mchakato wa uhawilishaji wa mawazo ama ujumbe wa maandishi kutoka katika utamaduni wa lugha chanzi na kuuweka ujumbe unaolingana nao katika utamaduni wa lugha lengwa (taz. Catford, 1965; Newmark, 1988). Aidha, Catford (1965:20) anasisitiza ulinganifu wa mawazo ya lugha chanzi katika lugha lengwa, anasema kufasiri ni kuchukua mawazo yaliyo katika maandishi kutoka lugha chanzi na badala yake kuweka mawazo yanayolingana na hayo katika lugha lengwa. Mtazamo wa wataalamu hawa umejikita hasa katika kutimiza kuwepo kwa ulinganifu wa maana na ujumbe uliopo kwenye matini chanzi na ule wa matini lengwa. Hii inamaanisha mfasiri anapokabiliwa na shughuli ya kutafsiri hana budi kutafuta visawe linganifu ambavyo ni sawa na vile vya matini chanzi na maana ya ujumbe.

Mwansoko (1996), anaielezea tafsiri kuwa ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo au ujumbe wa ulio katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Aidha, Mwansoko anasisitiza kuwa, tafsiri ndilo daraja linalounganisha jamii mbalimbali za watu wanaotumia lugha zinazotofautiana. Kadhalika, ni nyezo ya kueneza utamaduni, falsafa, maarifa na fasihi kutoka jamii moja hadi nyingine. Mawazo ya Mwansoko yanajenga msingi kuwa, kupitia tafsiri binadamu huweza kuingiliana na kutangamana katika maeneo mbalimbali ulimwenguni kwa kiasi kikubwa wakiwezeshwa na tafsiri za lugha. Mawazo ya wataalamu hao kuhusu dhana ya tafsiri yanashadadiwa na Huanga na mwenzake (2022) ambao wanaeleza kuwa tafsiri inahusisha uhamishaji wa mawazo au ujumbe ulio katika maandishi kutoka lugha chanzi kwenda katika lugha lengwa (Munday, 2018; Scott, 2018; Warwal, 2018; Jahan, 2023).

Jilala (2014a) anasisitiza kuwa, ili tafsiri ifanyike kwa ufanisi mfasiri hana budi kuwa na ujuzi wa lugha chanzi na lugha lengwa, utamaduni wa lugha hizo, isimu yake, sarufi na ujuzi wa kitaaluma katika tafsiri. Kwa hiyo, ulinganifu wa mawazo, utamaduni na vipengele vya lugha ndiyo mambo muhimu ya kuzingatiwa katika tafsiri (Jilala, 2023). Hivyo basi, kufanya tafsiri ni kuhusisha tamaduni mbili za jamiilugha zinazofanyiwa kazi; na kutafsiri siyo tu ni kushughulikia lugha bali ni pamoja na kushughulikia utamaduni wa lugha hizo (Reynolds, 2020). Hii ni kutokana na ukweli kwamba, maana na ujumbe wa maneno hujikita katika uelewa wa utamaduni wa jamii inayotumia lugha husika (Jilala, 2014a, Malangwa, 2014).

Aidha, katika kuelezea dhima ya tafsiri, Newmark (1988) na Mwansoko (1996) wanakubaliana kuwa, tafsiri ndilo daraja la mawasiliano ambalo linaunganisha jamii mbalimbali za watu wanaotumia lugha tofauti. Ni njia ya mawasiliano, na nyenzo ya kueneza utamaduni kutoka jamii moja hadi nyingine. Ni mbinu mojawapo ya kujifunza lugha za kigeni na ni kiliwazo cha nafsi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

## DHANA YA FASIHI LINGANISHI

Wellek (1988) anaielezea fasihi linganishi kuwa ni taaluma ya fasihi, nje ya mipaka ya kitaifa; ni kujifunza uhusiano uliopo baina ya fasihi na eneo jingine la maarifa, mathalani sanaa, falsafa, historia ya sanaa za jamii, sayansi na dini. Anasisitiza kuwa, fasihi linganishi ni ulinganishi wa fasihi na fasihi nyingine au nyinginezo na ulinganishi wa fasihi na mzunguko wa maisha ya binadamu. Kwa upana wa fasili hii tunaona kuwa Wellek anaiona fasihi linganishi katika misingi ya kiulinganishi inayohusisha vitu viwili. Kwamba unapofikiria fasihi linganishi basi huna budi kuwa na kazi mbili za fasihi ambazo unafikiria kuzilinganisha. Mawazo haya ni tofauti na yale ya Guyard ambaye ameitazama fasihi linganishi katika misingi ya kihistoria zaidi.

Aidha, kwa upande wake, Bassnett (1993) anaiona fasihi linganishi kuwa ni taaluma ya usomaji matini za tamaduni tofauti ili kubaini mazingira zinapokutana na zinapoachana. Nao Wellek na Warren (1996) wanaielezea fasihi linganishi kuwa ni mbinu itumiwayo na wahakiki wengi wa fasihi, hata wanasayansi, kujadili njia maalumu ya usomaji wa sanaa mbalimbali ulimwenguni.

Wataalamu kama vile: Damrosch (2020); Li (2022); Jahan (2023); na Ma Xiaolu (2024) wanakubaliana kuwa fasihi linganishi ni fasihi isiyokuwa na mipaka. Wanaendelea kueleza kuwa, fasihi ambayo inachunguza fasihi nje ya mipaka ya kitaifa na kimataifa. Inalinganisha kazi za fasihi za mataifa na lugha mbalimbali duniani. Na kupitia fasihi linganishi, watu hueweza kuelewa kuhusu jamii zingine, falsafa zao, itikadi, mielekeo na kaida na desturi zao.

Vilevile, Wamitila (2003) anaielezea fasihi linganishi kuwa, ni mbinu ya kuchunguza, kuchambua na kuelezea sifa za mfanano zilizopo katika matini ya fasihi; dhana hii huenda pamoja na dhana ya ulinganuzi. Ulinganuzi ni dhana ya kuchunguza, kuchambua na kuonesha sifa zinazotofautiana baina ya matini zaidi ya moja za kifasihi. Kwa maana hiyo, ulinganishi na ulinganuzi sharti uzingatie fani na maudhui. Kutokana na fasili hii, tunabaini kuwa, fasihi linganishi si tendo tu la kulinganisha bali ni kulinganisha na kulinganua kazi za fasihi ili kuibua kufanana na kutofautiana kwa kazi hizo kifani na kimaudhui.

Kwa upande wake Jilala (2016) anaeleza kuwa, fasihi linganishi ni taaluma inayojishughulisha na ulinganishaji wa kazi za fasihi na sanaa nyingine. Fasihi linganishi ni taaluma ya kulinganisha na kulinganua. Hii ina maana kuwa, unapolinganisha ndipo unapolinganua kazi zaidi ya moja. Ni taaluma inayoshughulikia tofauti au kufanana kwa fasihi ya makundi mawili au zaidi ya kiisimu, kiutamaduni, kihistoria, kiitikadi, kiuchumi, kijamii na kimataifa. Anaendelea kusema kuwa, kwa kutumia taaluma hii, tunaweza kulinganisha kazi za fasihi za lugha tofauti. Mfano, fasihi ya Kichina, Kijerumani, Kijapani, Kifaransa, Kiingereza, Kiswahili na nyinginezo, lakini bado inajishughulisha na fasihi ya lugha moja ikiwa kazi hizo asili yake ni nchi tofauti au utamaduni tofauti ndani ya lugha hiyo. Fasihi linganishi haijikiti katika ulinganishaji wa kazi za fasihi za nje ya nchi tu, bali ni taaluma inayoshughulikia ulinganishaji wa kazi za fasihi za nje na ndani ya nchi. Kwa mfano, ulinganishaji unaweza kuhusisha kazi za msanii mmoja, wasanii wawili au zaidi wanaoandika kwa kutumia lugha moja. Kwa mfano, unaweza kulinganisha kazi za fasihi za waandishi wa fasihi ya Kiswahili kama vile Kezilahabi na Shaaban Robert, Emmanuel Mbogo na Said Mohammed ama Ebrahim Hussein na Edwin Semzaba. Aidha, Jilala (2016) anaongezea kuwa ni taaluma inayoshughulikia ulinganishaji wa kazi za fasihi za msanii mmoja. Hii ina maana kwamba, unaweza kulinganisha kazi za fasihi zilizoandikwa na mtunzi mmoja. Kwa mfano, unaweza kulinganisha kazi za fasihi za Kezilahabi za vipindi tofauti. Mfano, kazi zake za miaka ya 70 na zile za miaka ya 90 ili kuibua mabadiliko yake katika usanii na sanaa ya utunzi ama mabadiliko ya mtazamo na falsafa yake katika ubunaji wa kazi za fasihi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

Hivyo, tunaweza kuhitimisha kuwa, fasihi linganishi ni taaluma inayohusika na ulinganishi wa kazi za fasihi za ndani na nje ya mipaka ya kitaifa, kibara na kilimwengu. Hii ina maana kwamba, kwa kutumia misingi na nadharia za fasihi linganishi tunaweza kulinganisha kazi za ndani ya nchi, nje ya nchi, bara moja na bara jingine na hata fasihi ya lugha moja na lugha nyingine, jamii moja na jamii nyingine na hata kazi za mwanafasihi mmoja za vipindi tofauti (Jilala, 2016).

Hivyo, baada ya kutalii dhana ya fasihi linganishi tumeona kuwa ni fasihi ambayo inahusisha ulinganishaji wa kazi za fasihi ndani na nje ya mipaka ya kitaifa, kibara na kilimwengu. Shughuli ya ulinganishaji haiwezi kufanyika bila kuwa na uelewa wa fani na maudhui ya kazi zinazozilinganishwa. Hivyo, makala hii inalenga kutathmini mchango wa tafsiri katika maendeleo ya fasihi linganishi ya Kiswahili. Katika kuangazia mchango wa tafsiri katika maendeleo ya fasihi linganishi, makala hii imelenga kubainisha umuhimu wa tafsiri na changamoto ya tafsiri katika fasihi linganishi. Aidha, katika makala hii tumetumia mifano ya kazi za fasihi ya Kiswahili na kazi za fasihi ya Kiingereza katika mjadala, ufafanuzi na urejelezi wa hoja za makala hii.

**Nadharia ya Utafiti**

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Usawe wa Kidhima ambayo iliasisiwa na Nida (1964) na baadaye kuendelezwa na Nida na Taber (2004) katika andiko lao kuhusu tafsiri ya Biblia liitwalo *The Theory and Practice of Translation*. Katika andiko hili wataalamu hawa wanasisitiza kuwa, katika usawe wa kidhima, tunashughulika na kuoanisha ujumbe na maana kati ya lugha chanzi na lugha lengwa. Aidha, Ponou (2013) na Fisher (2018) wanaeleza kuwa nadharia hii ni faafu kwa sababu inalenga kuwasilisha ujumbe asilia wa lugha chanzi kwa kadiri iwezekanavyo. Nadharia ya Usawe wa Kidhima inasisitiza kwamba, dhumuni la tafsiri ni kuleta athari ileile ya lugha chanzi katika lugha lengwa ili kuhakikisha hadhira inakuwa na mwitiko sawa au mguso sawa na hadhira ya lugha lengwa. Hivyo, mwitiko wa hadhira ya lugha chanzi uwe kama wa hadhira ya lugha lengwa. Ili kufikia lengo hili, mfasiri huchukua mawazo ya lugha chanzi na kuyahamisha katika lugha lengwa lakini si kwa muundo na mtindo ule ule bali kwa muundo na mtindo unaoleta athari na mwitiko sawa. Kwa mujibu wa Nida na Taber (2004) Nadharia ya Usawe Kidhima ina misingi minne ambayo ni; kutilia maanani usawe wa kidhima dhidi ya usawe wa kimundo. Pili, kuwa na mwelekeo wa kidhima kuliko wa kimuktadha. Tatu, kuzingatia umuhimu wa lugha inayosikika kuliko inayoandikwa. Nne, kuzingatia mahitaji ya hadhira kuliko muundo wa lugha. Misingi hii inatufaa katika utafiti huu katika kutathmini tafsiri yoyote ile huwa tunawalenga hadhira kuliko muundo wa lugha husika. Aidha, Nadharia ya Usawe wa Kidhima ina mihimili minne. Mosi, kuwa na usawe wa tungo baina ya LC[1] na LL[2]. Mhimili huu unaegemea zaidi katika LL. Pili, ujumbe wa LC uhawilishwe kwa njia inayoonesha uasili katika LL. Mhimili huu unataka tafsiri inayotolewa inapaswa isomeke kana kwamba imeandikwa katika lugha inayotolewa, haipaswi kuwa na vionjo vya LC. Tatu, kudumisha uhusiano baina ya ujumbe wa LC na ujumbe wa LL baaada ya tafsiri. Mhimili huu unaegemea zaidi katika kuziunganisha LC na LL. Nne, kuwa na mwitiko sawa kati ya hadhira ya LC na hadhira ya LL.

Kama tuvyoeleza, nadharia hii imetumika katika utafiti huu. Uteuzi wa nadharia hii umezingatia kuwa ni nadharia ambayo inasisitiza athari sawa ya ujumbe kwa hadhira ya matini chanzi na matini lengwa. Kwa hiyo, ili kuweza kulinganisha kazi za fasihi lazima hadhira zote mbili zipate athari iliyo sawa ya ujumbe na maana ya matini chanzi na matini lengwa. Hivyo, Nadharia hii ilituongoza katika kujadili changamoto za ulinganishaji wa kazi zilizotafiriwa na pia kujadili mchango wa tafsiri katika maendeleo ya fasihi linganishi.

[1] Lugha chanzi

[2] Lunga Lengwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

### Methodolojia ya Utafiti

Data za makala hii zilikusanywa kutoka maktabani. Hivyo, mbinu ya usomaji matini ilitumika kukusanya data zinazohusu matini za kifasihi zilizotafsiriwa, changamoto ya kutafsiri matini za kifasihi na mchango wa tafsiri katika fasihi linganishi kwa kuongozwa mkabala wa uchambuzi wa maudhui. Ili kufahamu vyema changamoto ya kutafsiri matini za kifasihi na mchango wa tafsiri katika fasihi linganishi, mtafiti alisoma tasnifu, vitabu na makala mbalimbali zinazohusu changamoto ya kutafsiri matini za kifasihi na mchango wa tafsiri katika fasihi linganishi kwa sababu vyanzo hivyo vya maarifa vimezungumzia kwa kina masuala hayo. Hivyo, mtafiti alipata maarifa kutoka katika vyanzo hivyo na kisha kutumia maarifa hayo kufanya uchanganuzi wa data. Mtafiti alisoma matini kwa kufuata hatua zifuatazo; Hatua ya kwanza ilikuwa ni kusoma kwa kina matini zilizotafsiriwa ili kubaini changamoto za kutafsiri matini za kifasihi. Hatua ya pili ilikuwa kusoma tena kwa kina sehemu zinazohusu mchango wa tafsiri katika fasihi linganishi. Hatua ya tatu ilikuwa kusoma tena matini ili kuweka alama kwenye maelezo yanayohusu mchango wa tafsiri na changamoto ya kutafsiri matini za kifasihi. Hatua ya nne ilikuwa kusoma tena kwa kina sehemu zilizozungumzia mchango wa tafsiri na changamoto ya kutafsiri matini za kifasihi ili kuhakiki kama ni maelezo na mifano inaendana na data. Baada ya hapo, uchambuzi wa data ulifuata.

## MCHANGO WA TAFSIRI KATIKA MAENDELEO YA FASIHI LINGANISHI

Kazi za fasihi ni zao la jamii ambalo pia huwasilisha utamaduni, mila, kaida, desturi, mitazamo, itikadi na mielekeo ya jamii kuhusu malimwengu yao na mazingira yanayowazunguka (Mwansoko, 1996:42). Anaendelea kueleza kuwa tafsiri hutumika kama nyenzo ya kuyahamisha hayo yote katika lugha ya utamaduni mwingine. Tazama nukuu ifuatayo kutoka kwa Mwansoko

Kwa vile fasihi huchukuliwa kuwa ni kioo cha jamii matini za kifasihi daima hushindiliwa dhana kemkem za kiutamaduni. Mfasiri anayeamua kufasiri kazi yoyote ya kifasihi ni lazima aufahamu vema utamaduni wa jamii inayotumia lugha chanzi na pia ule wa jamii inayotumia lugha lengwa na aweze kuziwianisha ipasavyo tamaduni hizo. Pasipokuwepo na uwiano wa kiutamaduni tafsiri hukosa maana ya mawasiliano na itabakia kuwa ni tafsiri ya kiisimu.

Kwa maana hiyo, ni dhahiri kuwa tafsiri ni taaluma muhimu katika kuelewa fasihi linganishi ya ulimwengu. Kama kiunganishi na daraja linalounganisha jamii za lugha na tamaduni tofauti, tafsiri ina umuhimu mkubwa katika ulinganishaji wa kazi za fasihi. Umuhimu wa tafsiri katika fasihi linganishi ni: Kusaidia kufahamu fasihi ya ulimwengu, kutajirisha fasihi ya jamii, kuwezesha na kufanikisha ulinganishaji, maendeleo ya nadharia za fasihi linganishi, maendeleo ya mbinu za kifani katika kazi za fasihi, maendeleo ya kimaudhui, huwezesha mawasiliano, tafsiri ni nyenzo ya kufunza na kueneza utamaduni wa jamii ulimwenguni, kubainisha misingi na kanuni za utunzi wa fasihi ya ulimwengu. Sehemu ifuatayo inajadili umuhimu wa tafsiri katika taaluma ya fasihi linganishi.

### Kusaidia kufahamu fasihi ya ulimwengu

Ili kuweza kuelewa fasihi ya ulimwengu katika ulimwengu wa utandawazi tafsiri inatumika kama nyenzo na daraja la mawasiliano na utambuzi wa fasihi za jamii mbalimbali (Constantinescu, 2017; Bassnett, 2018; Lun, 2018; Huanga, na mwenzake, 2022; Jahan, 2023). Huanga, na mwenzake (2022) wanasisitiza kuwa, huwezi kulinganisha vitu viwili ambavyo huvitambui na huelewi maarifa na misingi yake. Hivyo, ili kufanikisha ulinganishaji wa kazi zilizotafsiriwa, tafsiri hutusaidia kuweza kujua kile kinachowasilishwa na fasihi ya jamii nyingine kifani na kimaudhui na pia maarifa na uelewa huu huwa ni mwongozo wa ulinganishaji wa kazi hizo. Naye Lun (2018: 392) anaeleza kuwa, katika maendeleo ya fasihi linganishi, tafsiri imechukua

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

sehemu muhimu zaidi. Bila tafsiri, fasihi ya pande zote, uelewa na mawasiliano hayawezi kupatikana; bila bidii ya mfasiri, fasihi linganishi haiwezi kufanyika. Anaendelea kusisitiza kuwa, katika tafsiri ya fasihi, mfasiri pia hutumika kama mwandishi wa fasihi. Kazi yake ya sanaa ina ushawishi mkubwa katika fasihi ya lugha lengwa. Anatolea mfano wa tafsiri ya kifasihi ya Lin Shu, ambayo alitafsiri kazi kama vile *The Lady of Camellias*, *The Cabin of Uncle Tom*. Kazi hizi zilipanua upeo wa kusoma na kuandika kwa Kichina, na zilichangia katika ukuaji na maendeleo ya riwaya za kisasa za Kichina. Lun (Amekwishatajwa), anatoa mfano wa Zhu Shenghao, ambaye alijitolea kutafsiri kazi za Shakespeare. Alianza kutafsiri kazi hizo mwaka 1935, na miaka kumi iliyofuata, alikuwa tayari ametafsiri juzuu 27. Tafsiri ya kazi hizo za kifasihi iliwaletea wasomaji wa Kichina kazi za mwandishi Shakespeare mwandishi maarufu wa tamthiliya kutoka Uingereza, na hivyo kuimarisha fasihi ya Kichina.

**Kutajirisha Fasihi**

Tafsiri husaidia kutajirisha fasihi ya lugha ama taifa fulani. Na katika utajiri huo, basi watu huweza kulinganisha fasihi yao na fasihi ya lugha nyingine kupitia tafsiri. Kazi zinapotafsiriwa, zinafahamika na watu wanapata uelewa na maarifa ya fani na maudhui ya kazi hizo na kurahisisha shughuli za ulinganishaji. Lun, (2018: 392) anadhihirisha hili kwa kusema bila tafsiri fasihi linganishi haiwezekani. Hii ina maana kwamba huwezi kulinganisha fasihi ya Kichina na Kiarabu kama hazipo katika lugha unayoifahamu. Aiello (2005: 101) anaeleza kuwa, baadhi ya kazi za mahashumu Shaaban Robert zimeshatafsiriwa kwa Kirusi. Kusanyiko la kazi hizi linaitwa *Moya zhizn* kwa Kirusi, yaani "Maisha Yangu". Chapisho la kwanza lililotolewa katika mwaka wa 1968 lilihusisha tafsiri za vitabu vya Shaaban Robert kama vile *Kusadikika*, *Adili na Nduguze*, *Maisha yangu*, *Wasifu wa Siti Binti Saad* pamoja na insha zake nyingine. Aidha chapisho la pili lilitolewa mwaka 1981 kwa tafsiri ya Kirusi. Chapisho hili linaitwa kwa Kirusi *Izbran noye* kumaanisha "Kazi Teule" (Zhukov, 1998:185). Hili lilihusisha tafsiri ya *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*, *Siku ya Watenzi wote*, *Utubora Mkulima* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Tafsiri za kazi hizi ni dhahiri kuwa zimetajirisha fasihi ya Kirusi kutokana na kazi hizo kutumika kuziba pengo la mahitaji ya kazi za fasihi kwa nyakati husika.

Tafsiri imefanya kazi kubwa ya kutajirisha na kuchochea ufahamu wa fasihi ya Kiswahili na fasihi zingine duniani. Huko juu tumeona kazi mbalimbali zilizotafsiriwa kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili na kazi hizo kuwa ni hazina katika fasihi ya Kiswahili. Aidha, zipo baadhi ya kazi za fasihi ya Kiswahili ambazo zimetafsiriwa kwa lugha zingine na hivyo kufanya mataifa mengine kuelewa kuhusu fasihi ya Kiswahili.

**Kuwezesha na Kufanikisha Ulinganishaji**

Tafsiri ni kiungo muhimu katika fasihi linganishi. Ni dhahiri kuwa, bila tafsiri, fasihi linganishi isingewezekana na pia ulimwengu usingeweza kubadilishana maarifa na ujuzi mbalimbali ( Jahan, 2023; Ma Xiaolu, 2024). Pia, ulimwengu pia usingeweza kubadilishana na kuiga tamaduni za jamii mbalimbali (Mehrpouyan na mwenzake, 2021; Li, 2022; Ma Xiaolu 2024). Hii ni kwa sababu, tafsiri hufunua yaliyomo katika fasihi ya jamii moja na kuzifanya jamii nyingine ziweze kuelewa fasihi hiyo. Kuwezesha uelewa na ufahamu wa maarifa ya kifani na kimaudhui ya kazi za fasihi za jamii fulani, maisha yao, itikadi, falsafa, siasa, uchumi na utamaduni wa jamii hiyo. Uelewa huu huwezesha mlinganishaji kuweza kulinganisha fasihi hiyo na fasihi ya lugha yake kwa urahisi. Mehrpouyan na mwenzake (2021:18) wanaeleza kuwa, mustakabali wa fasihi linganishi hutegemea masomo ya tafsiri. Wanaongezea kuwa, watu hulinganisha na kulinganua kazi za fasihi kupitia tafsiri. Anatolea mfano wa washairi wa Iran kama vile Hafez, Saadi na Molana ambao sio tu Wairani maarufu sana ambao wanajua kusoma na kuandika pia wanajulikana sana duniani kote kutokana na

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

tafsiri za kazi zao katika lugha mbalimbali. Fauka ya hayo, baadhi ya watafsiri kama vile Najaf Daryabandari, Mohammad Sobhani, Mohammad Ghazi na wengineo wanatambulika vyema nchini Iran kutokana na tafsiri za kitaalamu. Katika fasihi ya Kiswahili, kazi tafsiriwa kama vile *Barua Ndefu Kama Hii* (Fasihi ya Senegali) *Mfalme Edipode* (Fasihi ya Kigiriki), *Mabepari wa Venisi* (Fasihi ya Kiingereza), *Julias Kaizari* (Fasihi ya Kiingereza) na zinginezo zinaweza kulinganishwa na kazi za fasihi ya Kiswahili. Ulinganishaji huu unawezekana kwa sababu zimetafsiriwa na zipo katika lugha ya Kiswahili. Mfano, Jilala (2016) aliweza kulinganisha tamthiliya ya *Mashetani* na *Mfalme Edipode*. Katika ulinganishaji huo alibaini kuwa kazi hizi mbili zinafanana zote zinawasilisha dhamira ya Ukombozi.

**Maendeleo ya Nadharia za Fasihi Linganishi**

Tafsiri imetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nadharia za fasihi linganishi ya Kiswahili. Kama tulivyoeleza hapo juu maendeleo ya nadharia ya fasihi linganishi yanahitaji kuwepo kwa tafsiri iliyo faafu. Hivyo, tafsiri ya kazi za fasihi zilizotajwa hapo awali zimesaidia kukuza na kuendeleza nadharia ya fasihi linganishi kinadharia na kivitendo. Aidha, watafiti na wanazuoni wameweza kufanya tafiti na kuandika vitabu na makala mbalimbali kuhusu fasihi linganishi kutokana na maarifa na taarifa walizozipata kupitia tafsiri. Kwa mfano, Ponera (2014) katika kitabu chake cha *Kitangulizi cha Fasihi Linganishi* anafafanua kuhusu nadharia ya fasihi linganishi. Jilala (2016) katika kitabu chake cha *Fasihi Linganishi: Nadharia Mbinu na Matumizi* anaelezea na kufafanua kuhusu nadharia za fasihi linganishi katika muktadha wa Kiswahili. Katika kitabu hicho amefafanua nadharia na matumizi ya nadharia kama vile nadharia ya athari na uigaji, nadharia ya mwingilianomatini, nadharia ya upokezi na namna zinazotumika katika fasihi linganishi. Kimsingi, Ponera na Jilala kupitia machapisho yao wameweza kuchangia katika maarifa ya fasihi linganishi na maendeleo ya fasihi linganishi ya Kiswahili. Ni dhahiri kuwa, tafsiri imechangia maendeleo ya fasihi linganishi hususani ufahamu na uelewa wa nadharia hizo na matumizi yake. Aidha, Lun (2018) anathibitisha kuwa tafsiri imesaidia katika maendeleo ya fasihi linganishi ya Kichina pia Ma Xiaolu (2014) amesema tafsiri ilisaidia kupeleka fasihi ya Kirusi nchini China na kuathiri fasihi ya Kichina.

**Maendeleo ya Mbinu za Kifani**

Tafsiri imechangia katika kuhamisha mbinu za kifani kutoka jamii moja kwenda jamii nyingine na kutoka kwa mwandishi mmoja wa kazi ya fasihi kwenda kwa mwandishi mwingine. Kazi za fasihi zilizotafsiriwa kutoka katika lugha za Kiingereza na Kilatini zilisaidia kukuza na kuimarisha mbinu za kifani za watunzi wa fasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, watunzi wa tamthiliya za Kiswahili walipata maarifa kutoka kwa maarufu kama vile Shakespear. Miongoni mwa watunzi hao ni Emmanuel Mbogo ambaye alithibitisha kuathiriwa na mtindo na mbinu za utunzi wa tamthiliya zilizotumiwa na watunzi kama Shakespear (Jilala, 2016). Aidha, Jilala (2004:81) anaeleza kuwa utunzi wa Emmanuel Mbogo hususani matumizi ya mbinu na matumizi ya sitiari, jazanda, kejeleli, tashtiti, muundo na kadhalika ni matokeo ya athari aliyoipata kwa kusoma vitabu vya tamthiliya za Shakespeare zikiwemo zile zilizotafsiriwa na J.K. Nyerere za *Mabepari wa Venisi (1969)* na *Juliasi Kaizari (1963)*. Emmanuel Mbogo anathibitisha kuwa, ilikuwa kazi ngumu kwake kusoma na kuelewa vitabu vya Shakespeare vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Lakini kupitia tafsiri za vitabu hivyo zilizofanywa na J.K. Nyerere zilimpa mwanga na uelewa zaidi katika kutunga tamthiliya zenye ujumi uliokomaa. Kwa mfano, ni utunzi wa kazi zake za *Morani* (1993) na *Sundiata* (2009) umetokana na athari na uigaji wa utunzi na ubunifu wa tamthiliya za Shakespeare, Racine, Soyinka na Gaethe. Tamthiliya ya *Fumo Liyongo* ina athari ya *Mackbeth* ya Shakespeare.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

**Maendeleo ya Kimaudhui**

Maendeleo ya kimaudhui hususani falsafa, dhamira, na mielekeo ya kijamii imeweza kukua kupitia tafsiri. Kwa mfano, Jilala (2016) alilinganisha tamthiliya ya Mashateni na Mfalme Edipode. Ulinganishaji huu umefanikiwa kwa sababu ya tafsiri. Tamthiliya ya kitanzia *Oedipus The King* iliandikwa na Sophocles (427 K.K) na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Samueli S. Mushi (1971). Katika ulinganishaji huo anajadili kuwa, tamthiliya zote mbili zinajadili kuhusu dhamira za ukombozi, mapinduzi, usariti, na mapenzi. Tofauti za tamthiliya hizi inatokana na mabadiliko ya wakati katika kanuni na taratibu za utunzi, mazingira, muktadha na wakati ambao huamua ni aina gani ya mtindo wa kazi za fasihi unafaa kwa kipindi hicho. Anaeleza kuwa, *Mfalme Edipode* (1971) ni tamthiliya ya Kiaristotle wakati tamthiliya ya *Mashetani* ni ya Kiafrika inayotumia mbinu za uingizaji wa vipengele vya fasihi simulizi za Kiafrika katika utunzi wake. Aidha, katika ulinganishaji huo Jilala (2016) anahitimisha kuwa fasihi za kilimwengu zinafanana na kutofautiana kwa sababu binadamu wote wana mahitaji yaliyo sawa na hivyo hatua za maendeleo ya binadamu ni kiini cha maendeleo ya fasihi.

**Tafsiri Huwezesha Mawasiliano**

Kama alivyoeleza na Mwansoko (1996) kuwa tafsiri ni daraja la mawasiliano. Hivyo, katika fasihi linganishi tafsiri ina dhima ya daraja la mawasiliano kwa sababu tafsiri huwezesha mawasiliano baina ya jamii za lugha tofauti. Kupitia kazi ya fasihi iliyotafsiriwa, mlinganishaji huweza kuelewa ujumbe na maana ya kazi za fasihi za jamii nyingine na hivyo kuweza kuzilinganisha na fasihi ya lugha yake. Tafsiri huwezesha mawasiliano baina ya matini na mlinganishaji ili kuweza kufahamu ujumbe na maana zinazotumika katika kazi za fasihi za jamii nyingine. Kwa mfano, kitabu cha ushairi cha *Song of Lawino* ambacho kilitafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili kama *Wimbo wa Lawino*. Tafsiri hii imesaidia jamii ya Waswahili kufahamu ujumbe, mila, desturi, kaida na mambo mengine ambayo yamezungumziwa katika *Song of La*wino. Hivyo, kupitia uelewa huu ni rahisi kwa mlinganishaji kulinganisha kitabu cha *Song of Lawino* na kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, unaweza kulinganisha na shairi la *Mwanakupona* na kuonesha jinsi fani na maudhui ya kazi hizo mbili yanavyofanana na kutofautiana. Na hivyo kuwasaidia wasomaji wa kazi zote mbili kuelewa na kupata mawasiliano ya ujumbe na maana iliyokusudiwa katika matini chanzi. Aidha, tafsiri iliyofanywa na Aiello ambaye ametafsiri riwaya ya *Utengano* (1980) ya mwandishi S.A. Mohamed kwa lugha ya Kiitaliano na ambayo ilichapishwa mwaka 2005 na kuitwa *Separazione* (Aiello, 2005: 104). Tafsiri hii pia inasaidia mawasiliano kwa wasomaji wa lugha zote mbili na ni rahisi mlinganishaji wa fasihi ya Kiitaliano kulinganisha kazi ya fasihi ya Kiitaliano na kitabu cha Kiswahili cha *Utengano*. Maelezo haya pia yamebainishwa na watafiti wengine kuhusu namna tafsiri inavyosaidia kuwezesha mawasiliano katika fasihi linganishi (taz. Carlos, 2012; Constantinescu, 2017; Lun, 2018).

**Tafsiri ni Nyenzo ya Kueneza Utamaduni**

Tafsiri imetoa mchango mkubwa katika kueneza utamaduni kutoka jamii moja hadi jamii nyingine (Munday, 2016) . Tumekwishaeleza kuwa, zipo matini nyingi za fasihi ambazo zimetafsiriwa kutoka katika lugha za Kiafrika kwenda katika Kiingereza pia kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha za Kiafrika na lugha nyingine duniani. Katika ulimwengu wa teknolojia na utandawazi tunaona jamii zikishirikiana katika fasihi kwa kutumia mbinu ya tafsiri. Kwa mfano, kazi za sanaa ya filamu kutoka katika fasihi ya Kihindi, Kituruki, Kikorea na Kichina zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na kurushwa katika televisheni mbalimbali kama vile Azam Two, Azam one, ITV, TBC, Swahili *boolyhood* na nyinginezo. Harakati hizi zinafungua njia ya kufahamu fasihi ya jamii nyingine, utamaduni wao, uzoefu wao, mifumo na mielekeo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

kiutamaduni. Ufahamu huo unatoa nafasi kwa jamii kujitazama, kujikosoa, kujilinganisha na jamii nyingine na hata kuiga tamaduni mpya ambazo hazipo katika jamii.

Aidha, inasaidia kufahamu mazingira ya jamii nyingine na historia zao na namna wanavyoyakabili malimwengu yao. Kwa kufahamu hilo, inasaidia katika kuiga na hata kuchota mbinu zinazotumiwa na jamii nyingine kuyakabili mazingira yao na kuzitumia katika muktadha wa jamii zetu. Aiello (2005) akimnukuu Bertoncini-Zubkova (2004), anaeleza kwamba wapo wanafunzi wa Kiitaliano ambao tayari wametafsiri kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili katika tafiti zao. Baadhi yao wananuia kuchapisha kazi hizo kwa lugha ya Kiitaliano. Bila shaka huu ni mchango mkubwa katika hazina ya fasihi tafsiri ya Kiswahili. Hatua hii itachangia kueneza fasihi za Afrika Mashariki sio tu barani Ulaya bali pia katika mataifa mengine ulimwenguni. Aiello (2005:103) anaeleza kwamba kutafsiri kazi bunifu za Kiswahili kwa Kiitaliano kutafungua ukurasa mpya na kupata wasomaji wengi zaidi wa kazi hizo. Hii ni njia moja ya kusambaza utamaduni wa Kiswahili kwa mataifa mengine ulimwenguni.

Baadhi ya riwaya za Kiswahili pia zimefanyiwa tafsiri kwa lugha za kigeni. Mifano ni kama vile riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi (1978) na ambayo ilitafsiriwa kwa Kifaransa na Karthala na kuchapishwa kwa anuwani *Les gerofliers de Zanzibar* mnamo mwaka 1986. Baadaye riwaya hii ilitafsiriwa upya na Serpent Plumes mwaka wa 2000 na kuitwa *Die Sklaverei der Gewurze* (Aiello, 2005:100-101). Hivyo, tafsiri hizo zinasaidia katika maendeleo ya fasihi linganishi. Hii ni kwa sababu ni rahisi kwa jamii chanzi na jamii lengwa kuweza kulinganisha fasihi zao kifani na kimaudhui. Kwa mfano, ni rahisi kwa jamii ya Wafaransa kulinganisha fasihi yao na fasihi ya Zanzibar na hivyo kujifunza utamaduni wa Mzanzibar na maisha yao. Ni rahisi pia kwa Waitaliano kulinganisha fasihi yao na fasihi ya Kiswahili kwa sababu kazi hizo za fasihi zipo katika lugha yao.

### Mbinu ya Kujifunza na Kufundisha Lugha ya Kigeni

Tafsiri husaidia kujifunza lugha ya jamii nyingine. Mfasiri anapotafsiri kazi ya fasihi ya lugha nyingine, kwanza yeye mwenyewe hujifunza lugha hiyo na kuongeza misamiati mipya hasa pale anapotumia kamusi kujua istilahi mbalimbali ambazo zimetumika katika lugha anayoifanyia kazi. Vilevile, husaidia kuelewa matumizi ya tamathali za semi, misemo, methali na nahau za lugha mpya. Hivyo, uelewa wa lugha na mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha husaidia katika ulinganishaji wa kazi za fasihi, kuweza kuonesha kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya lugha katika kazi za fasihi zinazolinganishwa. Kwa mujibu wa Ruhumbika (1983), tafsiri za fasihi za kigeni ni njia mojawapo ya kuikuza fasihi ya Kiswahili. Hivyo, fasihi iliyotafsiriwa husaidia katika kuinua kiwango cha ubora katika uwasilishaji wa fasihi ya Kiswahili. Aidha, tafsiri hizo zinakuwa ni nyenzo za kujifunza lugha ya kigeni na kujifunza miundo na maumbo ya lugha nyinginezo za kigeni. Kwa wafasiri wa fasihi, inakuwa ni njia mojawapo katika kuupanua msamiati. Wanaotafiti lugha na utamaduni wa jamii ngeni huweza kuanzia katika fasihi tafsiriwa na baadaye kulinganisha na fasihi asili ili kuimarisha kiwango chao cha mawasiliano na wenyeji.

### Tafsiri Inakuza na Kueneza Lugha

Tafsiri ina dhima ya kukuza na kueneza lugha katika jamii mbalimbali. Tafsiri ya kazi mbalimbali za fasihi husaidia kueneza lugha kupitia mchakato wa kuhamishia miundo ya misemo, sarufi na maana za maneno ya lugha chanzi kwenye lugha lengwa (Munday, 2016; Lun, 2018). Hivyo, uelewa huu humwezesha mlinganishaji anapolinganisha kazi za tafsiri kuweza kulinganisha mtindo wa matumizi ya lugha, miundo ya misemo, tamathali za semi na maana za maneno yaliyotumika katika kazi moja ya fasihi na kazi nyingine. Kwa mfano, tafsiri za kazi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

za tamthiliya kutoka katika lugha za Kichina, Kikorea, Kihindi na Kituruki kwenda katika lugha ya Kiswahili zinasaidia hadhira ya lugha chanzi kujifunza lugha ya Kiswahili na pia lugha za kigeni.

## CHANGAMOTO ZA KULINGANISHA KAZI TAFSIRIWA

Ulinganishaji wa matini za kifasihi ambazo zimetafsiriwa huwa na matatizo na changamoto zake. Baadhi ya wataalamu wa tafsiri wameeleza kuwa matini za fasihi hutatiza mno zinapolinganishwa na matini nyingine (Nord, 2005; ). Endapo mfasiri hatazingatia mbinu za kutafsiri matini za kifasihi anaweza kuzalisha tafsiri ya kifasihi ambayo haina ulinganifu wa ujumbe na maana iliyokusudiwa katika matini chanzi. Hivyo, iwapo tafsiri itakosewa ni dhahiri kuwa uzito wa ujumbe uliokusudiwa katika matini chanzi hupoteza uzito na hata kuifanya matini kuwa ya kawaida (Malmkjær, 2020). Vilevile, unaweza kupotea ushikamani na matini chanzi. Kwa maana hiyo, mlinganishaji wa matini ya tafsiri hukutana na matini ambayo tayari ni zao la matini ya lugha chanzi na si matini asilia. Hivyo, iwapo tafsiri ya kazi ya fasihi ina matatizo na inapotosha maana na ujumbe asilia basi huathiri ulinganishaji. Kwa hiyo, ulinganishaji wa kazi za fasihi zilizotafsiriwa hukumbana na matatizo kama vile; Tofauti za kiutamaduni, tofauti za kimtindo na mbinu za kisanii, baadhi ya matini kukosa ushikamani wa maana na ujumbe, baadhi ya matini kukosa ushikamani wa kimuundo na kimtindo, baadhi ya matini kukosa ujumi wa kisanii, na matini za tafsiri kukosa mvuto wa kisanii.

### Tofauti za Kiutamaduni

Kila lugha ina utamaduni wake ambao ni tofauti na utamaduni wa jamii nyingine. Utamaduni huu hufungamana na fasihi ya jamii hiyo kwa sababu mtunzi hutumia malighafi ya jamii kujenga kazi yake kifani na kimaudhui. Kwa msaada wa tafsiri tunafahamiana na kufahamu desturi, kanuni za mavazi, na utamaduni wa nchi nyingine. Kwa mfano, uteuzi wa lugha kama vile tamathali za semi, misemo, nahau na methali zinazotumika katika kazi ya fasihi hufungamana na mila, desturi, historia, mazingira, muktadha na wakati. Hivyo, kazi za fasihi zinapotafsiriwa hukumbana na changamoto ya tofauti za kiutamaduni na mfasiri asipoweza kuzitambua na kuzikabili tofauti hizi huweza kupotosha maana na ujumbe wa kazi ya fasihi. Upotoshaji huu huathiri ulinganishaji wa kazi za fasihi kwa sababu kile kinachozungumzwa katika matini chanzi ni tofauti na kile kinachowasilishwa katika matini lengwa. Tofauti ya lugha chanzi na lugha lengwa huweza kuathiri ulinganishaji wa kazi za fasihi (Lun, 2018). Tazama mifano kutoka katika tamthiliya ya *Mabepari wa Venisi* iliyotafsiriwa na Julius Kambarage Nyerere:

| **MC[3]- Kiingereza** | **ML[4]- Kiswahili)** |
|---|---|
| But we will visit you at supper time | Walakini tutakuja kwako saa za kula jioni |
| Sir, I entreat you home with me to **dinner** | Bwana, karibu nyumbani kwa **chakula cha jioni** |

**Chanzo:** *Mabepari wa Venisi* (1969)

Ukichunguza mifano hiyo utabaini kuwa utamaduni wa Kiingereza hutumia neno ‘*Supper*’ na ‘*dinner*’ kurejelea dhana mbili tofauti. ‘*Supper*’ ni mlo wa usiku, ilhali ‘*dinner*’ ni mlo mkuu wa siku na aghalabu huliwa kuanzia saa 6 mchana na kuendelea. Dhana hizi ni tata kufasiriwa kwa usahihi katika Kiswahili, ambapo jamii ya Waswahili kwa kawaida ina milo mitatu tu kwa siku: kifungua kinywa, chakula cha mchana, na chakula cha jioni (Mwansoko, 2016). Kwa hiyo,

[3] Matini Chanzi

[4] Matini Lengwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

changamoto ya tofauti za kiutamaduni inaweza kuathiri ulinganishaji wa kazi za fasihi ambazo zina maudhui yaliyojengwa kwa kutumia dhana zinarejelea milo. Hii ni kwa sababu Waswahili wana dhana tatu zinazolejerea milo tofauti na Waingereza ambayo hufikia hadi mitano: breakfast, lunch, high tea, dinner, supper.

**Tofauti za Kimtindo na Mbinu za Kisanii**

Kazi za fasihi zilizotafsiriwa huwa na changamoto ya tofauti za kimtindo. Mfasiri anapotafsiri anaweza kushindwa kuhamisha mtindo wa matini chanzi katika matini lengwa. Hivyo, wakati wa kulinganisha kazi ya aina hii mlinganishaji hulinganisha kazi ambayo tayari ina matatizo ya kimtindo na hivyo huweza kuathiri ulinganishaji (Lun, 2018). Kwa mfano, tafsiri ya *Wimbo wa Lawino* iliyofanywa na Sozigwa (1975) ya kitabu cha mwandishi Okot p ‘Bitek *Song of Lawino* (1966) inadhihirisha hilo. Tazama mfano ufuatao hapa chini.

| **MC - Kiingereza** | **ML -Kiswahili** |
|---|---|
| The stomach seems to be | Inaonekana tumbo lina |
| A powerful force | Nguvu kubwa |
| For **joining** political parties | **Inayounganisha** vyama vya siasa |
| Especially when the purse | Hasa kama pochi iliyo |
| In the trouser pocket | Katika mfuko wa suruali |
| Carries only the coins | Inabeba mapeni tu. |

Katika tafsiri hii kitenzi “joining” kimetafsiriwa kwa utenge kuwa “inayounganisha” badala ya “kuingia” au “kujiunga” na hivyo, kupotosha maana ya ubeti wa LC. Kwa hiyo, upotoshaji wa maana huweza kuathiri ulinganishaji wa kazi ya fasihi. Mlinganishaji, hulinganisha ujumbe ambao si sahihi.

**Upotoshaji wa Maana**

Katika tafsiri, changamoto ya upotoshaji wa maana hujitokeza pale ambapo matini chanzi inapopotoshwa kwa kutumia mbinu ambayo si sahihi ama utuezi wa visawe visivyo sahihi. Kwa mfano, baadhi ya tafsiri hufanyika kwa kutafsiri dhana za matini chanzi kwa kutumia mbinu ya ujumuishaji. Ambapo dhana kadhaa hutafsiriwa kwa kutumia neno moja. Tazama, mifano ifuatayo kutoka katika *Song of Lawino (1966) ‘Wimbo wa Lawino (1975)*.

| 1. **MC: Kiingereza** | **ML: Kiswahili** |
|---|---|
| Witches | Wachawi |
| Sorcerers | Wachawi |
| Herbalists | Wachawi |
| 2. Primitive | Mshamba |
| Uneducated | Mshamba |
| Unbaptized | Mshamba |
| Uncivilized | Mshamba |

Ukichunguza mifano hiyo utaona maneno ya Kiswahili ‘Mchawi’ na ‘Mshamba’ yametumika kutafsiri dhana zaidi ya moja za Kiingereza. Katika lugha ya Kiingereza dhana zilizorejelewa hapo juu zina maana tofauti, na wala sio maana moja kama inavyopendekezwa katika tafsiri ya Kiswahili. Mifano mingine ni tafsiri ya: Things Fall Apart kutafsiriwa kama Shujaa Okonkwo, Merchant of Venice kutafsiriwa kama Mabepari wa Venis, *The Trials of Dedan Kimathi* ‘Mzalendo Kimathi’ na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

*Dying in the Sun* 'Kivuli Kinaishi'. Tafsiri hizi zinaonesha kuna tatizo la ulinganifu wa visawe. Mlinganishaji anapolinganisha kazi hizi na kazi zingine za fasihi anaweza kupotosha ujumbe na dhamira za kazi za fasihi hizo. Kwa sababu maana ya jina la kitabu imepotoshwa. Kwa mfano, mfasiri wa Merchants of Venice ametafsiri neno Merchant kama Mabepari badala ya Wafanyabiashara hii ni kutokana na kuwa muumini wa falsafa ya ujamaa mbao ndo mfumo uliokuwa ukiongoza Tanzania katika miaka ya 1970 – 1980 (TUKI, 2005). Tafsiri hii inaonesha jinsi mfumo wa ubepari ambao ni wa kinyonyaji ulivyokuwa haukubaliki katika jamii ya LL katika miaka hiyo. Tazama mfano namba 3 kutoka katika *Wimbo wa Lawino* tafsiri ya *Song of Lawino*.

| 3. | **MC- Kiingereza** | **ML- Kiswahili** |
|---|---|---|
| | First take a deep look, brother.<br>You are now a man<br>You are not **a dead fruit**<br>To behave like a child does not<br>Befit you! | Kwanza jifikirie sana, ndugu<br>Sasa wewe ni mtu mzima<br>Wewe si **embe bovu**<br>Kufanya vitendo kama mtoto mdogo<br>Si mahali pako |

Katika mfano namba tatu hapo juu mfasiri amefasiri **a dead fruit** kama **embe bovu**. Tafsiri hii inapotosha maana na ujumbe wa matini chanzi kwa sababu katika matini chanzi mtunzi alimaanisha tunda lakini katika matini lengwa mtunzi ametumia embe. Pembe (2010) anasema embe ni tunda kuu na linalothaminiwa sana katika jamii ya Kizaramo anakotoka mfasiri; kwa hiyo, mfasiri aliathiriwa na mazingira ya utamaduni wake ndio maana akafasiri hivyo. Tafsiri hii inaweza kuathiri ulinganishaji kwa sababu ya upotoshaji wa maana ya matini chanzi katika matini lengwa.

**Ukiukaji wa Mbinu za Kisanii**

Uhawilishaji wa mbinu za kisanii huwa ngumu kutafsirika. Matini za kifasihi husheheni mbinu za kisanii ambazo zinaambatana na matumizi ya tamathali semi kama vile sitiari, taswira, tashihisi, tashibiha au nahau. Hivyo, tafsiri ya matini za kifasihi huwa ngumu kwa mfasiri kuhawilisha mbinu za kisanii kutoka lugha moja kwenda lugha nyinine. Tamathali hizo huweza kutafsiriwa kwa kutumia lugha ya kawaida ama kudondoshwa. Hivyo, tafsiri za Kiswahili za fasihi ya kigeni hupoteza ladha na vionjo vya kisanii na kuonekana chapwa (Mwansoko, 2016). Tazama mifano ifuatayo kutoka katika Mabepari wa Venisi:

| **MC- Kiingereza** | **ML- Tafsiri ya Kiswahili** |
|---|---|
| And when I open my lips,<br>let no **dog** bark. | Nitapoanza kusema,<br>kila **mtu** anyamaze! |

Ukichunguza mfano huo, utaona kwamba katika matini chanzi neno 'dog' limetumika kisitiari na kutafsiriwa kwa lugha ya kawaida katika matini lengwa kama 'mtu'. Tafsiri imeondoa usitiari wake. Tafsiri hii haina ulinganifu wa visawe na hivyo inaweza kuathiri ulinganishaji wa kazi ya fasihi. Kwa mfano, mlinganishaji anapotumia matini tafsiriwa anaweza kusema lugha iliyotumika ni ya kawaida wakati matini chanzi imetumia lugha ya sitiari. Hiyo, mlinganishaji anapokutana na hali kama hii hupotosha ulinganishaji kwa sababu ya upotoshaji uliofanyika katika tafsiri. Tazama mfano ufatao kutoka katika *Wimbo wa Lawino*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

| **MC-Kiingereza** | **ML- Kiswahili** |
|---|---|
| Maria **the clean woman** | Maria Mtakatifu |
| Mother of the **Hunchback** | Mama wa Mungu |
| Pray for us | Utuombee |
| **Who spoil things** | Sisi wakosefu |
| Full of Graciya | Uliyejaa neema |

Katika data hiyo, tunaona kwamba mfasiri ametumia lugha nyepesi na ya kawaida ukilinganisha na matini chanzi ambayo msanii ametumia lugha ya kejeli dhidi ya dini ya Kikristo iliyoletwa na Wazungu na hivyo kuzikandamiza imani asilia za Waafrika, haionekani kabisa kwenye matini ya Kiswahili. Mwandishi wa MC alitumia maneno "*the clean woman*", "*Hunch back*" na *'who spoil things*' kwa makusudi ili kubeza Ukristo. Tafsiri ya Kiswahili, kwa upande wake, imeonekana kuutukuza Ukristo, kinyume kabisa na lengo la mwandishi wa MC.ama anavyobainisha Mtesigwa (1996: 89) katika uchambuzi wake wa tafsiri ya kitabu cha *Wimbo wa Lawino*, anasema tafsiri ya Kiswahili ni ya kiungwana mno na imepoa sana ikilinganishwa na MC. Kwa hiyo, matini tafsiri hii inaonesha kuwa hakuna ulinganifu wa visawe na hakuna athari iliyo sawa baina ya matini chanzi na matini lengwa. Kwa hiyo, mlinganishaji anapokutana na matini ya aina hii huweza kupotosha fani na maudhui ya matini iliyotafsiriwa wakati wa ulinagnishaji wa kazi za fasihi kutokana na upotoshaji uliojitokeza katika tafsiri. Wilt (2003), anasema kuwa watafsiri wengi wanajua kuwa jazanda na tamathali nyingine za jamii moja haziwezi kuhamishwa moja kwa moja bali kuna haja ya kuteua visawe vya kiuamilifu na visawe rasmi. Uteuzi wa visawe rasmi unatoa visawe ambavyo haviendani na muktadha wa matumizi. Kutokana na hoja hii, mtafsiri anaweza kuteua visawe vya kiuamilifu ambavyo vitaweza kuwasilisha ujumbe. Mtafsiri huwa na kazi ya ziada kutafuta visawe ambavyo vitamsaidia kuwasilisha ujumbe wa matini chasili kikamilifu pasipo kuutatiza kwa njia yoyote ile. Wakati mwingine tamathali zinapotafsiriwa hupotosha ujumbe na kama mtafsiri atakosa uangalifu, tafsiri mbovu itatatiza uwasilishaji wa ujumbe kutoka matini chasili hadi matini tafsiri.

## HITIMISHO

Makala hii imejadili mchango wa tafsiri katika maendeleo ya fasihi linganishi. Makala imejadili kuwa tafsiri ina uhusiano mkubwa wa tafsiri na fasihi linganishi hasa kama daraja kuu la ulinganishaji na uelewa wa fasihi za kiulimwengu. Katika makala hii tumeona kuwa tafsiri ni taaluma ambayo haiwezi kutenganishwa na taaluma ya fasihi linganishi. Tunapojikita katika mkabala wa kuitazama fasihi linganishi kama taaluma nje ya mipaka ya kitaifa na kimataifa, hatuwezi kuepuka tafsiri. Kwa sababu, tafsiri ndiyo kiungo na mhimili wa ulinganishaji wa matini za kifasihi za jamii na utamaduni tofauti; jamii ambazo zinatofautiana kiitikadi na kifalsafa katika namna ya kuyatazama maisha na malimwengu yao. Ni dhahiri kwamba taaluma ya tafsiri na fasihi linganishi ni taaluma mbili zenye uhusiano wa kiutegemezano. Kwa hiyo, iwapo tafsiri itakuwa tenge basi ulinganishaji wa fasihi linganishi utakuwa tenge kwa kupotoka kimaana na kisarufi. Kufanya hivyo, kutasaidia kuwa na tafsiri sahihi za kifasihi na kurahisisha ulinganishaji ambao utaleta matokeo bora.

Makala hii imeonesha umuhimu wa tafsiri katika maendeleo ya fasihi linganishi kwa kujadili kuwa kutajirisha fasihi ya jamii, kuwezesha na kufanikisha ulinganishaji, maendeleo ya nadharia za fasihi linganishi, maendeleo ya mbinu za kifani katika kazi za fasihi, maendeleo ya kimaudhui, huwezesha mawasiliano, tafsiri ni nyenzo ya kufunza na kueneza utamaduni wa jamii ulimwenguni, kufahamu fasihi ya ulimwengu, kubainisha misingi na kanuni za utunzi wa fasihi ya ulimwengu. ulinganishaji wa kazi za fasihi zilizotafsiriwa hukumbana na matatizo kama vile;

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

Tofauti za kiutamaduni, tofauti za kimtindo na mbinu za kisanii, baadhi ya matini kukosa ushikamani wa maana na ujumbe, baadhi ya matini kukosa ushikamani wa kimuundo na kimtindo; baadhi ya matini kukosa ujumi wa kisanii na matini za tafsiri kukosa mvuto wa kisanii.

**MAREJELEO**


Aiello, F. T. (2005). Translating a Swahili Novel into 'Kizungu'. *Swahili Forum 12. pgs. 99-107*

Damrosch, D. (2020). *Comparing the Literatures*. Princeton, NJ: Princeton University Press.

Bassnett, S. (1993). *Comparative Literature*: *A Critical Introduction*, Oxford UK & Cambridge USA: Blackwell.

Bassnett, S., ed. (2018). *Translation and World Literature*. New York: Routledge.

Baaqeel, N. (2018). Would Comparative Literature be replaced by Translation Studies? *Annals of Language and Literature*, 2(4), pp. 18-25.

Bitek, O.P. (1966). *Song of Lawino*. Nairobi: East African Educational Publishers Limited.

Carlos, G. (2012). Towards A New and More Constructive Partnership: The Changing Role of Translation in Comparative Literature. *Tee Fu Jen Studies*, vol. 45

Catford, J.C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University.

Constantinescu, M. C. (2017). The Role of Translation in Comparative Literature: Conjectures and Solutions. *Finnish Journal for Romanian Studies*. No. 3. 12-23.

Huanga, Q., and Valdeóna R. A. (2022). Perspectives on translation and world literature. *PERSPECTIVES*. 30 (6), 899– 910 https://doi.org/10.1080/0907676X.2022.2132062

Jahan, F. (2023). Comparative Literature and Translation Studies: Approaching an Understanding Between the Two. *International Journal of Social Science and Human Research, 6 (3),1582-1588.*

Jilala, H. (2014 b). *Athari za Kiutamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii katika Makumbusho za Tanzania*. Tasnifu ya Uzamivu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Jilala, H. (2014 a). Matatizo ya Tafsiri katika Matini za Kitalii Nchini Tanzania. Katika Omari S na Peterson (wah.). *Kioo cha Lugha*. Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Juz. No.12 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. kur. 27-47.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi.* TUKI & Daud Publishing Company LTD.

Jilala. H. (2023). Mchango wa Tafsiri za J.K. Nyerere katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili. *Jarida la Mwanga wa Lugha*. 8 (1) .75-88.

Nyerere, J.K. (1969). *Mabepari wa Venisi*. Dar es Salaam, OUP.

Kelly, L.G (1979), *The True Interpreter: A History of Translation, Theory and Practice In the West*, Bristol: Basil Blackwell.

Knappert, J (1979), *Four Centuries of Swahili Verse*, London: Leiden.

Li, X. A. (2022). Translation and comparative literature. In K. Malmkjaer (Ed.), *The Cambridge Handbook of Translation* (pp. 217–237). Cambridge University Press.

Lun, W. (2018). The Essence of Literary Translation in Comparative Literature. *Advances in Social Science, Education and Humanities Research*, volume 250, 391-394

Ma Xiaolu (2024). Cultural Brokerage: Japan as an Intermediary in the Journey of Russian

Article DOI : https://doi.org/10.37284/eajass.8.1.2652

Literature to China. *Modern Language Association of America*. Cambridge University Press. 139 (2), 267-281.

Malangwa, P.S. (2014). "Challenges of Translating Cultural Expressions in Teaching Kiswahili to Foreigners" katika *Kiswahili*, Dar es Salaam, TUKI, juz. 771 104-117.

Malmkjær, K. (2020). *Translation and Creativity*. London: Routledge.

Mehrpouyan, A and Zakeri, E. (2021). The Impact of Cultural and Translational Studies on

Modern Comparative Literature Studies. *International Journal of Linguistics, Literature and Translation.*

Munday, J. (2016). *Translation Theory: Introducing Translation Studies: Theories and Applications.* 4th ed. New York, NY: Routledge.

Momanyi. C. (2017). Tafsiri za Fasihi ya Kiswahili na Mchakato wa Utandawazi. *Mulika*. 32.

Mtesigwa, P.C.K. (1996). "Kitabu cha Wimbo wa Lawino kama Tafsiri na kama Tafsiri ya Ushairi", katika Mwansoko, H.J.M. *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*, Dar es Salaam, TUKI: 84-96.

Mwansoko, H.J.M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*, Dar es Salaam: TUKI.

Mwansoko, H.J.M (2016). "Dhana, Dhima na Historia ya Tafsiri" katika Jilala, H (mh.). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Daud Publishing Company Ltd. Kur. 2-17

Newmark. P. (1988). *A Textbook of Translation*. London, Prentince Hall.

Nord, C. (2005). *Text Analysis in Translation: Theory, Methodology and Didactic Application of A Model for Translation-Oriented Text Analysis*. (toleo la 2). New Jersey: Rodopi B.V. Amsterdam-New York.

Nyerere, J.K. (1963). *Juliasi Kaizari*, Nairobi, OUP.

Nyerere, J.K. (1969). *Mabepari wa Venisi*, Dar es Salaam, OUP.

Pembe, H. (2010). *The Challenges of Translating Poetic Text: The Case of Paul Sozigwa's Wimbo wa Lawino*, Tasnifu ya Shahada ya Umahiri ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Karjamer Printing Technology, Dar es Salaam.

Reynolds, M., ed. (2020). *Prismatic Translation*. Cambridge: Legenda.

Ruhumbika, G. (1983). "Tafsiri za Kigeni katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili" katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI, kur. 253- 266.

Scott, C. (2018). *The Work of Literary Translation*. Cambridge: Cambridge University Press.

Sozigwa, P. (1975). *Wimbo wa Lawino.* Dar es Salaam: East Africa Publishing House.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Focus Publication Ltd.

Warwal, S. S. (2018). Role of Translation in Comparative Literature. *Translation today*. 40-60.

Wellek, R. (1988). *"The Crisis in Comparative Literature." Concepts of Criticism*. Ed. Stephen G. Nichols, Jr. New Haven: Yale UP. 282-95.

Wellek, R. & Warren, A. (1996). *Theory of Literature*. New York: Brace and Company.

Zhukov, A. (1998). Shaaban Robert in the Russian Language. *Swahili Forum 5. Pgs. 185-189*

 | This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License